TANGAZO LA SERIKALI Na. 62 la tarehe 31/1/2025

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 106 (1) (bb))*

KANUNI ZA UDHIBITI WA MATUMIZI YA MSUMENO WA MOTO ZA MWAKA 2025

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
USAJILI WA MSUMENO WA MOTO

4. Usajili wa msumeno wa moto.
5. Mabadiliko ya taarifa za msumeno wa moto.

SEHEMU YA TATU
UDHIBITI WA MATUMIZI YA MSUMENO WA MOTO

6. Kibali cha matumizi ya msumeno wa moto.
7. Masharti ya kibali.
8. Kufutwa kwa kibali.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

9. Rufaa.
10. Adhabu ya jumla.

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

---

## KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 106(1)(bb))*

KANUNI ZA UDHIBITI WA MATUMIZI YA MSUMENO WA MOTO ZA MWAKA 2025

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Udhibiti wa Matumizi ya Msumeno wa Moto za Mwaka 2025.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto katika ukataji miti ya asili au ya kupandwa kwenye eneo lolote.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"msumeno wa moto" maana yake ni msumeno wa mnyororo unaoendeshwa kwa kutumia mashine kukatia miti.

Sura ya 323

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Misitu;

TS. Na 269 la 2010

"Kamishna wa Uhifadhi" maana yake ni Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania.

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya misitu.

## SEHEMU YA PILI
## USAJILI WA MSUMENO WA MOTO

Usajili wa msumeno wa moto

**4**.-(1) Mtu hataruhusiwa kutumia msumeno wa moto ambao haujasajiliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu ambaye anakusudia kutumia msumeno wa moto, atasajili msumeno huo kwa kuwasilisha maombi kwa Kamishna wa Uhifadhi.

(3) Maombi ya usajili wa msumeno wa moto yatawasilishwa kupitia Fomu Na.1 kama ilivyoainishwa katika ya Jedwali la Kanuni hizi, yakiambatishwa na-

(a) kitambulisho cha muombaji; na
(b) uthibitisho wa umiliki wa msumemo wa moto unaoombewa usajili;

(4) Kamishna wa Uhifadhi atapaswa kushughulikia maombi yaliyowasilishwa kwake ndani ya siku saba tangu kupokea maombi hayo, na baada ya kujiridhisha na maombi hayo anaweza-

(a) kukubali maombi na kusajili msumeno wa moto kwa kumpatia muombaji cheti cha usajili kama kilivyoainishwa katika Fomu Na. 2 ya Jedwali la Kanuni hizi; au
(b) kukataa maombi hayo na kumjulisha muombaji sababu kwa maandishi.

Mabadiliko ya taarifa za msumeno wa moto

**5**.-(1) Mtu anayemiliki msumeno wa moto uliosajiliwa anaweza, wakati wowote baada ya usajili, kuwasilisha kwa Kamishna wa Uhifadhi maombi ya mabadiliko ya taarifa za usajili wa msumeno wa moto kama ilivyoainishwa katika Fomu Na. 3 ya Jedwali la Kanuni hizi.

(2) Maombi ya mabadiliko ya taarifa za usajili wa msumeno wa moto yanaweza kujumuisha taarifa kuhusu-

(a) mabadiliko ya umiliki wa msumeno wa moto uliyosajiliwa;
(b) mabadiliko ya eneo la matumizi ya msumeno wa moto uliyosajiliwa;
(c) upotevu wa msumeno wa moto uliyosajiliwa; au

(d) jambo lolote lingine muhimu ambalo Kamishna wa Uhifadhi anaweza kuhitaji baada ya kupokea maombi hayo.

(3) Ikiwa maombi ya mabadiliko ya taarifa chini ya kanuni ndogo ya (2) yanahusisha upotevu wa msumeno wa moto, mwombaji atatakiwa kuambatisha taarifa ya upotevu inayotolewa na mamlaka husika.

(4) Baada ya kupokea maombi chini ya kanuni ndogo ya (3), Kamishna wa Uhifadhi atatakiwa kuhuisha taarifa hizo kwenye rejesta ya usajili na kumpatia mwombaji cheti cha usajili.

## SEHEMU YA TATU
## UDHIBITI WA MATUMIZI YA MSUMENO WA MOTO

Kibali cha matumizi ya msumeno wa moto

**6**.-(1) Mtu hatapaswa kutumia msumeno wa moto kwa shughuli za ukataji miti katika eneo lolote isipokuwa kwa kibali kinachotolewa na afisa mfawidhi wa wilaya mwenye dhamana ya usimamizi wa misitu.

(2) Maombi ya kibali chini ya kanuni ndogo ya (1) yatawasilishwa kwa kutumia Fomu Na. 4 iliyopo katika Jedwali la Kanuni hizi, na maombi hayo yataambatana na nyaraka zifuatazo:

cheti cha usajili wa msumeno wa moto; na

mkataba wa ukodishaji, iwapo msumeno wa moto unaoombewa kibali unamilikiwa na mtu mwingine.

(3) Baada ya kupokea maombi ya kibali na kujiridhisha na uhalali wa taarifa zilizowasilishwa, afisa mhifadhi wa wilaya anaweza-

kutoa kibali cha kutumia msumeno wa moto kama kilivyoainishwa katika Fomu Na. 5 ya Jedwali la Kanuni hizi; au

kukataa maombi hayo na kumjulisha muombaji sababu kwa maandishi.

(4) Afisa mhifadhi wa wilaya atatakiwa kuwasilisha kwa Kamishna wa Uhifadhi, taarifa ya vibali vya msumeno wa moto vilivyotolewa kila baada ya miezi mitatu.

Masharti ya kibali

**7**.-(1) Mmiliki wa kibali cha kutumia msumeno wa moto katika eneo lolote hataruhusiwa:

kuhamisha matumizi ya kibali hicho kwenda kwa mtu mwingine.
kutumia msumeno wa moto kupasua mbao.

Kufutwa kwa kibali

**8**.-(1) Kamishna wa Uhifadhi anaweza kufuta kibali kilichotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi endapo-
kibali kilipatikana kwa njia ya udanganyifu; au
mwenye kibali amekiuka masharti yoyote ya Sheria au Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), endapo mwenye kibali atasitishiwa kibali chake chini ya kanuni ndogo ya 1(b), Kamishna wa Uhifadhi anaweza akarejesha kibali endapo aliyesitishiwa kibali atakua amekidhi masharti ambayo yalikiukwa awali.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

Rufaa

**9**- (1) Mtu ambaye hataridhika na uamuzi wowote uliofanywa chini ya Kanuni hizi anaweza kukata rufaa-
kwa Waziri iwapo uamuzi huo umetolewa na Kamishna wa Uhifadhi; na
kwa Kamishna wa Uhifadhi iwapo uamuzi huo umetolewa na afisa mhifadhi wa Wilaya.

(2) Rufaa chini ya kanuni ndogo ya (1) itawasilishwa kwa njia ya maandishi ndani ya siku thelathini tangu tarehe ambayo uamuzi ulitolewa.

(3) Baada ya kupokea rufaa, Waziri au Kamishna wa Uhifadhi ataifanyia kazi rufaa hiyo na kutoa uamuzi kwa njia ya maandishi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupokea rufaa hiyo.

Adhabu ya jumla

**10**. Mtu atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi endapo atatiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

JEDWALI

*(Imeandaliwa chini ya kanuni ya 4(2) )*

FOMU NA. 1

Na. ……...

MAOMBI YA KUSAJILI MSUMENO WA MOTO

Mimi ......................................................................................... wa anwani ......................................... na namba ya simu.................................. naomba kusajili msumeno wa moto kwa ajili ya ukataji/uvunaji wa miti.

Taarifa kuhusu msumeno wa moto utakaosajiliwa:

1. Mahali msumeno utakapotumika (Wilaya):.............................................
2. Chapa (brand): ...................................
3. Aina (model): ...................................
4. Namba ya utambuzi(serial number): ..........................
5. Tarehe ya ununuzi: ............................
6. Uwezo wa injini (horsepower): ................................
7. Urefu wa msumeno: .............................

Jina na sahihi ya Mwombaji: ................................ Tarehe: .............................

FOMU NA. 2
*Na. ……..*

*(Imeandaliwa chini ya Kanuni ya 4(3)(a) )*

CHETI CHA USAJILI WA MSUMENO WA MOTO

Cheti hiki kimetolewa kwa .......................................................... (jina la mmiliki) wa .......................... (anwani), kutumia msumeno wa moto kwa shughuli za ukataji/uvunaji miti kama ifuatavyo;

1. Wilaya ambapo msumeno wa moto utatumika: ...............................
2. Chapa (brand): ........................Aina(model): ..........................
3. Tarehe ya ununuzi: ..................Namba ya utambuzi: .........................
4. Uwezo wa injini (horsepower): .........................
5. Urefu wa msumeno: ..........................
6. Tarehe ya kutolewa: ..................................

______________________ ___________________
(*Jina la muidhinishaji*) (*Cheo*)

Mahali: ___________________ Tarehe: __________________

FOMU NA. 3

*Na. ……...*

(*Imeandaliwa chini ya kanuni ya 5(1))*

MAOMBI YA KUBADILI /UMILIKI /ENEO LA MATUMIZI YA MSUMENO WA MOTO.

Mimi...................................................................... ...wa...............................................(anuani) ninaye miliki msumeno wa moto wenye namba za usajili .. .....................katika wilaya ................................naomba kubadili taarifa za umiliki/ eneo la matumizi ya msumeno wa moto.

1. Jina la mmiliki wa awali: __________
2. Jina la mmiliki mpya: __________
3. Wilaya ambapo msumeno utatumika: __________

Sababu za kubadili umiliki / Eneo la matumizi ...............................
Nathibitisha kuwa maelezo niliyotoa hapo juu ni sahihi.

__________ __________
(*Saini*)

Mahali: ___________________ Tarehe: ____________________

FOMU NA. 4
Na. ……...

(Imeandaliwa chini ya kanuni ya 6(2))

MAOMBI YA KIBALI CHA MATUMIZI YA MSUMENO WA MOTO

Mimi/..........................................................................wa..........................................(anwani) ninaye miliki msumeno wa moto wenye namba za usajili .. .....................wilaya ..................................naomba kutumia msumeno wa moto kwa shughuli za ukataji/uvunaji miti.

| S/N | NAMBA YA USAJILI WA MSUMENO WA MOTO | ENEO LA UKATAJI/UVUNAJI | NAMBA YA LESENI YA UVUNAJI | TAREHE YA UKOMO WA MATUMIZI YA LESENI YA UVUNAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

1. Jina la mwombaji ………………………………………………….
2. Namba ya simu………………………….
3. Tarehe…………………Saini ya Mwombaji ....…………………….

FOMU NA. 5
*Na. ……....*

*(Imeandaliwa chini ya kanuni ya 6(3)(a))*

KIBALI CHA MATUMIZI YA MSUMENO WA MOTO

Kibali kimetolewa kwa ……………………………………………. wa …............................... kutumia msumeno wa moto katika msitu/Eneo .....................Eneo/Mtaa ……………….. kama ifuatavyo;

1. Namba ya usajili wa msumeno wa moto ..................................
2. Namba ya leseni ya uvunaji .....................................
5. Mwisho wa matumizi wa kibali hiki ……………………….
6. Saini............................................
7. Tarehe ya kutolewa kibali .............................................

Jina la mtoaji..............................Cheo ...............................

Saini ........................ Tarehe ...................................

Dodoma,
16 Januari, 2025

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*